

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI OFISI YA MSIMAMIZI WA UCHANGUZI JIMBO LA MBEYA VIJIJINI



Kumb. Na. MDC/

21.09.2020

YAH: TANGAZO LA AJIRA YA USIMAMIZI WA UCHAGUZI KATIKA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2020

(Limetolewa chini ya Kanuni ya 14 ya Kanuni za uchaguzi wa Rais na wabunge, 2020 na Kanuni ya 12 kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani), 2020.

Msimamizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Mbeya Vijijini anayo furaha ya kutangaza nafasi za Ajira ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura, Wasimamizi wasaidizi wa vituo vya kupigia kura na Karani waongozaji wapiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28.10.2020.

1. WASIMAMIZI WA VITUO VYA KUPIGIA KURA – NAFASI 550

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania
- Awe na umri wa miaka 18 au zaidi
- Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha Siasa
- Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri

MAJUKUMU

1. Kusimamia zoezi la kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura, kutangaza matokeo ya Uchaguzi na kutuma matokeo husika kwa Msimamizi wa Uchaguzi.
2. Kupokea, kutunza na kuviwasilisha vifaa vya Uchaguzi, kwa Msimamizi wa Uchaguzi.
3. Kubandika matokeo ya Uchaguzi ya kituo kwenye Ubao wa matangazo.
4. Kushirikiana na Mawakala wa vyama vya Siasa ili kuhakikisha zoezi la upigaji kura linafanyika kwa amani, usalama na utulivu.
5. Kuhakikisha wapiga kura wanaopiga kura ni wale tu wenye kitambulisho cha mpiga kura na wamo kwenye daftari la kudumu la wapiga kura la kituo.
6. Kuandaa taarifa ya zoezi la uchaguzi kwenye kituo na kuiwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi.
7. Kushiriki katika Mafunzo ya Uchaguzi ili kufahamu taratibu za Uchaguzi.

2. WASIMAMIZI WASAIDIZI WA VITUO VYA KUPIGIA KURA – NAFASI 1,060

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa miaka 18 au zaidi.
- Awe ni mkazi wa Kata ambayo atafanya kazi ya kuongoza wapiga kura.
- Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu.
- Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuandika.
- Asiwe shabiki au kiongozi wa Chama cha Siasa.

MAJUKUMU

1. Kupokea wapiga kura ndani ya kituo siku ya uchaguzi.
2. Kukagua kadi ya mpiga kura ili kujiridhisha kama taarifa zake zinalingana na taarifa zilizomo kwenye daftari la kudumu la wapiga kura.
3. Kusoma kwa sauti jina la mpiga kura ili mawakala wa vyama vya siasa waliopo wamtambue mpiga kura.
4. Kuwaelekeza wapiga kura kutumbukiza karatasi za kupigia kura kwenye masanduku husika.
5. Kuhakikisha kuwa wapiga kura wote waliokwisha kupiga kura wanapakwa wino usiofutika kwenye kidole kidogo cha mwisho cha mkono.

3. KARANI WAONGOZAJI WAPIGA KURA - NAFASI 550

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa miaka 18 au zaidi.
- Awe ni mkazi wa Kata ambayo atafanya kazi ya kuongoza wapiga kura.
- Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu.
- Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuandika.
- Asiwe shabiki au kiongozi wa Chama cha Siasa.
- Awe tayari kumsaidia mpiga kura yeyote bila upendeleo wala ubaguzi wa namna yoyote.

MAJUKUMU


1. Kupokea wapiga kura nje ya kituo na kuwaelekeza eneo/chumba watakachopigia kura.
2. Atawaelekeza wapiga kura kujipanga katika mistari miwili yaani mstari wa wanawake na wanaume.
3. Kutoa kipaumbele kwa wapiga kura wenye mahitaji maalum kama vile watu wenye ulemavu, wagonjwa, wazee, wajawazito na akina mama wanaonyonyesha waliokuja na watoto wao vituoni.
4. Kushirikiana na watendaji wa kituo na mlinzi wa kituo katika kufanikisha kazi na upigaji kura kituoni.
5. Karani mwongozaji atawajibika kwa Msimamizi wa kituo cha kupigia kura.

4. MASHARTI YA JUMLA

- Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yaainishe kijiji na Kata Mwombaji anayoomba kusimamia Uchaguzi.

Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Mbeya Vijijini,
S.L.P 599,
MBEYA.

- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni siku ya Jumapili tarehe **27.09.2020** saa 10.00 jioni kwenye Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi Mbalizi Mji Mdogo.


Stephen E. Katemba
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA MBEYA VIJIJINI

